**KASSU 2022**
**MWONGOZO KISWAHILI**
**102/2**

MWONGOZO WA UFAHAMU

a)I) Okolo wakiwa wachanga walitumia harita siku hizi anakoga kwa sabuni
ii) Baragumu lilitumika katika mawasiliano, kijijini sasa wanajamii wana simu
2×1

b )
(i) Okolo anawafaa wanyonge na hawataki kumpigia kura
**(ii)** anasomesha mayatima wanadai yeye ni mwizi
**(iii)** anawapa mapeni wanadai ana mazingaombwe
**(iv)** babake aliwaalika wengi kwao wanamwita mamake maskini
**(v)** wanakijiji wanalenga aila tajiri ndizo zinafaa uongozi si maadili/maskini
**(vi)** Okolo anawajali majirani ilhali wengine waliofanikiwa majirani hawana haja/ wanaendeleza shughuli zao
(vii) Waliokasa kunywa pombe kuonekana wanyonge katika jamii
(viii) Okolo kuonja pombe udogoni nakumfanya afukuzwe shuleni japo anadai alilelewa vizuri.

Zozote 5×1

c)
**(i)** watu kusaidiana
**(ii)** burudani walifanya pamoja
**(iii)** wanasaidina kazi pamoja
**(iv)** Okolo anatumia gari lake kuwauni wagonjwa
**(v)** Kijiji cha Mulukoba ukarimu ulikuzwa
**(vi)** Wazee wanabugia pombe katika kikao chao
**(vii)** Kuna mfumo wa uongozi wa kidemokrasia

Zozote 4×1

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

d)
i) watoto kufiwa na wazazi-Okolo alifiwa na babake
ii) ugumu wa usafiri
iii) imani potovu-wengine wanadai ana mazingaumbwe
iv) ubinafsi-Okolo kujipata ndiye anajali hali ya watu/majirani zake Okolo wlijifaa wenyewe
v) Uhasama/chuki-wanakijiji wanapiga simu kutafuta kiini cha utajiri wa Okolo
vi) Masengenyo-Okolo anasengenywa na wenzake ati ni karimu/Ukarimu wake ni mada kijijini
vii) Dharau-mamake Okolo kudharauliwa ati ni muuza mboga tu.

e)
i) kuacha masomo. 2x1=2
ii) kukubali kushindwa.

**2 .Muhtasari - Mwongozo**

(a) Athari za mfumuko wa bei kwa wananchi

(i) Raia nchini wanalala njaa.
(ii) Wananchi kutumia nusu ya mapato yao kununua chakula
(iii) Gharama ya maisha imepanda.
(iv) Familia nyingi zimeingia katika lindi la umaskini.
(v) Wengi hawawezi kumudu bei ya bidhaa.

**(5x1=5, alama 1 utiririko)**

(b) **Mambo muhimu yanayozungumziwa na mwandishi**

(i) Serikali haina uwezo wa kudhibiti vyanzo vya ongezeko la bei.
(ii) Inapaswa kupanga mikakati fulani ili kukabiliana na hali hii.
(iii) Wanasiasa wanapiga siasa bila kujali maslahi ya kimsingi ya wananchi.
(iv) Baa la njaa limekuwepo na lipo nchini.
(v) Familia nyingi zimeathirika kwani zinashindwa kumudu bei ya bidhaa.
(vi) Serikali yapaswa kuchukua hatua ili kuhimili athari za mfumko wa bei.
(vii) Gharama ya kupangisha nyumba, maji, stima na mafuta imepanda.
(viii) Kupanda kwa bei ya vyakula imesukuma familia katika umaskini

**(8x1=8, alama 1utiririko)**

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

A. Andika neno lenye kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya mbele wastani, nazali ya midomo na irabu ya chini kati. (al. 2)
***Sema***

B. Bainisha uamilifu wa viambishi katika neno lifuatalo (al 2)
Viliwavyo
***vi-ngeli, iw-kauli/mnyambuliko, a –kiishio, vyo-kirejeshi***

C. Onyesha muundo ya silabi katika neno mbilikimo. (al 2)
***Mbi- kki, li-ki, ki-ki, mo-ki***

D. Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha A-unganifu, kitenzi kishirikishi kipungufu na kijalizo. (al 2)
***Wa mwalimu ni mchoyo(maneno yawe matatu pekee)***

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

E. Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi (al 2)
Mwanafunzi huyo akisoma kwa bidii atapita
***Wanafunzi hao wasiposoma kwa bidii hawatapita***

F. Ainisha vihusishi katika sentensi zifuatazo (al 2 )
i) Tunu ni mrembo kama mama yake
***kama -kilinganishi***
ii) Watawasili kufikia juma lijalo
***kufikia-wakati***

G. Tambua virai katika sentensi (al 2 )
Wenye bidii kazini wamesifiwa sana bungeni
***Wenye bidii kazini- RN Wamesifiwa sana bungeni –RT***

H. Tunga sentensi sahihi ukitumia kiunganishi cha kulinganisha (al 2 )
***kama, kuliko,sembuse / seuze***

I. Andika katika usemi wa taarifa (al 2 )
"Wanasiasa hawa wenu wakipigana hivi wataharibu nchi" Rais alisema
***Rais alisema kuwa/kwamba wanasiasa <u>hao wao</u> <u>wangeendelea</u> kupigana <u>hivyo</u> <u>wangeiharibu</u> nchi***

J. Changanua sentensi kwa jedwali (al 4 )
Jirani aliyenisaidia juzi ataondoka mwaka ujao.

| **S** | | | |
|---|---|---|---|
| **KN** | | **KT** | |
| **N** | **s** | **T** | **E** |
| **Jirani** | **aliyenisaidiajuzi** | **ataondoka** | **mwakaujao** |

K. Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo (al 3 )
Alawi alifumiwa mkeka mzuri na shangaziye kwa miyaa.
***mkeka mzuri-tendwa, Alawi-tendewa, miyaa-ala***

L. Tambua aina za vishazi katika sentensi (al 2)
Lazima nile lishe bora ili niwe mwenye afya.
***Lazima nile lishe bora-huru, ili niwe mwenye afya-tegemezi***

M. Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia vigezo viwili vikuu. (al 2)
Wanafunzi walikuwa wakiamka mapema
***muundo – sahili***
***dhamira – arifu/taarifa***

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

N. Bainisha maana mbili za sentensi ifuatayo (al 2 )
Mapunda alisema kuwa mkewe amesafiri.
***1.Mke wa Mapunda atasafiri 2.mke wa mtu mwingine atasafiri.***

O. Andika sentensi ifautayo katika wingi (al 1 )
Onyesha kivumishi katika sentensi ifuatayo
***Onyesheni vivumishi katika sentensi zifuatazo***

P. Geuza sentensi zifuatazo katika nyakati na hali katika mabano (al 2 )
i) Wanafunzi wanafanya mtihani ( ujao hali timilifu)
***Wanafunzi watakuwa wamefanya mtihani***
ii) Mtoto amekunywa maziwa (uliopita hali ya kuendelea)
***Mtoto alikuwa akinywa maziwa.***

Q. Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha miundo miwili ya ngeli ya U-ZI (al 2 )
***U-NY uzi-nyuzi, U-MB ubao-mbao, U-ND ulimi –ndimi,W-NY wembe –nyembe***

R. Tunga sentensi sahihi yenye kitenzi halisi.
Gari jipya ***limepita***
(al 1 )

S. Andika sentensi upya kulingana na maagizo (al 2 )
i) <u>Miti</u> ilikatwa <u>Nairobi</u> ( tumia viwakilishi vya maneno yaliyopigiwa msitari.
miti- ***hii,ile hiyo*** Nairobi – ***hapa pale hapo***
ii) Mtoto amekula wali ( geuza katika kauli ya kutendwa)
***Wali umeliwa na motto***

T. Onyesha matumizi ya KI katika sentensi hizi (al 2 )
i) Hakijapikiwa
***ngeli***
ii) Alinunua kimeza hafifu
***Udogo***

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

**ISIMUJAMII**

MTU 1: Una shida gani?
MTU 2: Kichwa chaniwanga, tumbo lanisokota na ninahisi uchovu mwingi. Nisaidie tafadhali.
MTU 1: Pole, afya yako itakuwa shwari. Hizi tembe hapa zitakusaidia kupunguza maumivu. Unapaswa kuzitumia mara tatu kwa siku…

i. Tambua sajili hii ( alama 2)
ii. Kwa kutolea mfano, andika sifa tatu ambazo zingetumika katika sajili hii( alama 3)

i) Umepewa jukumu la kuendesha shughuli ya mazishi kijijini mwako. Fafanua sifa tano za lugha utakayotumia wewe na waombolezaji wengine. (alama 5)

**MAJIBU**

a) **(i) sajili ya hospitalini- hizi tembe hapa zitakusaidia**

**(ii) matumizi ya tarakimu-Meza 1x3**
**Msamiati wa kitaaluma baina ya madaktari-TB**
**Kuchanganya ndimi-lab**
**Lugha nyepesi kwa mgonjwa ili aelewe**
**Lugha ya ishara-naumwa hapa.**
**Kadiria sifa nyingine ambazo hazipo kwenye muktadha**
**Zozote 3x1=3**

**b)**

**(i) Msamiati maalum wa mazishi, kwa mfano marehemu, waombolezaji**
**(ii) Sentensi ndefu ili kufafanua ili kwelewika**
**(iii) Lugha ya heshima- unapotambua waliohudhuria – kuitwa marehemu**
**(iv) Lugha legevu**
**(v) Kiimbo cha chini – kwa sababu ya kuombeleza**
**(vi) Takriri – Alikuwa mzuri, alikuwa mkarimu, marehemu**
**(vii) Sentensi fupi - mtuambee**
**(viii) Lugha ya maagizo-wenye magari waegeshe upande wa kushoto**
**(ix) Lugha ya kuliwaza – usife moyo**
**(x) Matumizi ya nyimbo – ili lukiwaza waliofiwa**

**Kila sifa iandamane na mfano mwafaka.**
**Bila mfano au maelezo mtahiniwa apate sufuri.**

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com